UHURU NA UMOJA

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA (TACAF)

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

# HUDUMA ZA MIKOPO

## UTANGULIZI

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umeanzishwa kwa sheria ya ujumuisho wa wadhamini (Trustees' incorporation Act) kama ilivyo rejelewa mwaka 2002 (CAP. 318 R.E.2023) na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 septemba, 2020.

## LENGO LA MFUKO

Kuinua ubora wa kazi za Utamaduni na Sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara, kutengeneza ajira nchini pamoja na pato la Taifa.

## SEKTA ZINAZO HUDUMIWA NA MFUKO

- Sanaa za Muziki - Taarabu, Injili, Singeli, Kizazi kipya, Kaswida, Hiphop, Muziki wa Dansi
- Sanaa za Filamu - Wazalishaji, Waandaaji wa Maudhui, Waigizaji, wasambazaji, waongozaji, wapiga picha, waandishi wa miswada, wana mandhali
- Sanaa za Maonesho - Upambaji, Sarakasi, Upishi, Michezo ya Jukwaani, U-DJ, Ushereheshaji, Ngoma za Asili
- Sanaa za Ufundi - Utengenezaji wa Batiki, Uchoraji , Ususi, uchongaji, Utengenezaji wa Shanga, Ubunifu wa mitindo, Uchoraji wa picha za Tingatinga
- Lugha na Fasihi - Waandishi wa vitabu, wasambazaji, watunzi wa mashairi

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

## WALENGWA WA MFUKO

- Mtu Binafsi;
- Kikundi; na
- Kampuni

## AINA YA HUDUMA ZA MKOPO

a) Mikopo ya uendeshaji:
Kuendesha kazi za walengwa kama vile matamasha, mashindano, kutayarisha au kuzindua kazi za Utamaduni na Sanaa na shughuli zingine zinazofanana na hizo.

b) Mikopo ya Vifaa
Kununua vifaa vya kazi vitakavyotumika katika kuzalisha kazi za Utamaduni na Sanaa.

c) Mikopo ya kujikimu / Dharura
Mikopo ya muda mfupu kwa ajili ya kujikimu wakati wa safari za kuandaa au kufanikisha kazi za Utamaduni na Sanaa

## VIGEZO VYA WANUFAIKA WA MKOPO KWA WAOMBAJI BINAFSI

- Barua ya maombi ya mkopo;
- Andiko la mradi wa biashara;
- Ankara Kifani ( endapo mkopo ni wa vitendea kazi).
- Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN);
- Leseni ya biashara kama ipo;
- Barua ya utambulisho wa eneo la biashara kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji;
- Picha mbili za mkopaji na Mwenza wake kama yupo;
- Uthibitisho wa vyanzo vingine vya mapato kama yapo;
- Kitambulisho cha Taifa/Hati ya Kusafiria/Leseni ya Udereva;
- Cheti cha usajili kutoka Taasisi inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya mwombaji kwenye Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa;
- Barua ya uthibitisho kuwa Mwombaji ni mwanachama wa Umoja wowote ikiwamo Shirikisho au Chama kilichosajiliwa kisheria katika Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa na ametambulishwa kwa maandishi na umoja huo;
- Uthibitisho wa mzunguko wa mapato na matumizi yatokanayo na kazi za Sanaa kupitia benki au miamala ya simu.

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

## VIGEZO VYA WANUFAIKA WA MKOPO KWA WAOMBAJI KAMPUNI

- Barua ya maombi ya mkopo;
- Andiko la mradi wa biashara;
- Ankara Kifani ( endapo mkopo ni wa vitendea kazi).
- Taarifa za hesabu zilizokaguiwa kwa mwaka mmoja;
- Picha mbili za Viongozi wa Kampuni;
- Leseni ya biashara;
- Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) na utakaso wa kodi ( Tax Clearence);
- Memorandum and Article of associations;
- Nakala ya mizania ya mwaka 'annual returns' iliyoidhinishwa na BRELA;
- Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wanamiliki wa Taasisi ukionesha mahitaji ya mtaji na kuafikia kuomba mkopo;
- Cheti cha usajili kutoka Taasisi inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya mwombaji kwenye Sekta ya Utamaduni na/au Sanaa;
- Barua ya uthibitisho kuwa Mwombaji ni mwanachama wa umoja wowote ikiwamo Shirikisho au Chama kilichosajiliwa kisheria katika Sekta ya

Utamaduni na/au Sanaa;

- Uthibitisho wa mzunguko wa mapato na matumizi yatokanayo na kazi za sanaa kupitia Benki au miamala ya simu.

## VIGEZO VYA WANUFAIKA WA MKOPO KWA WAOMBAJI KIKUNDI

- Barua ya maombi ya mkopo;
- Andiko la mradi wa biashara;
- Ankara Kifani ( endapo mkopo ni [illegible] ndea kazi).
- Picha mbili za Viongozi wa Ki[illegible]
- Leseni ya biashara;
- Nakala ya hati ya usajili;
- Muhtasari wa kikao ulios[illegible] w[illegible] achama wa kikundi wenye ajenda ya maom[illegible] kop[illegible]
- Barua ya uthibiti[illegible] ku[illegible] M[illegible] mbaji ni mwanachama wa Umoja wowote ikiwamo S[illegible] kisho au[illegible] kili[illegible] katika Sekta ya Utamadu[illegible] na/au Sa[illegible]
- Uthibitis[illegible] ma[illegible] na kazi za sa[illegible] pitia Benki [illegible] mala y[illegible]

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

## SIFA ZA MKOPO

- Kiwango cha Mkopo ni kuanzia TZS 200,000/= hadi 200,000,000/=
- Muda wa Marejesho ni miezi 36 (Miaka 3)
- Riba ni asilimia (9%).
- Muda wa rehema (grace period) ni miezi mitatu (3).

## NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:
Afisa Mtendaji Mkuu,
Mfuko wa Utamaduni na Sanaa,
S.L.P 8031,
DAR ES SALAAM

Na kuwasilishwa kupitia:
Barua pepe: mfuko.utamaduni@michezo.go.tz

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

MFUKO WA
UTAMADUNI NA
SANAA TANZANIA

Jengo la Utumishi,
Kitalu A, 8 Barabara ya Kivukoni,
11101 Kivukoni, Dar es Salaam.

0738 246 286/ 0738 246 315

*www.tacaf.go.tz*

mfuko.utamaduni@michezo.go.tz

mfukotamadunitz